**HOTUBA YA MWENYEKITI WA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI MHE. JAJI (R) (MST.) SEMISTOCLES S. KAIJAGE KWA WARATIBU WA UCHAGUZI WA MIKOA NA WASIMAMIZI WA UCHAGUZI TAREHE 17 OKTOBA, 2020**

- **Ndugu Waratibu wa Uchaguzi wa Mikoa**
- **Ndugu Wasimamizi wa Uchaguzi**
- **Watendaji kutoka Tume ya Uchaguzi,**
- **Wanahabari,**
- **Mabibi na Mabwana.**

**Tumsifu Yesu Kristo    Asalam Aleikum**

Napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia uzima na kutuwezesha kukutana siku ya leo katika mkutano huu muhimu. Umuhimu wa mkutano huu unatokana na jukumu kubwa tulilonalo la kuratibu na kusimamia uendeshaji wa Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani unaotarajiwa kufanyia tarehe 28 Oktoba, 2020. Sisi tuliopo hapa ndio watendaji tunaotegemewa kufanikisha jukumu hili.

Aidha, niwashukuru kwa kuitikia wito wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa kuhudhuria mkutano huu na niwape hongera kwa utekelezaji wa

majukumu mliyonayo na hasa jukumu hili la maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020.

**Ndugu Washiriki**

Kwa kuzingatia Ratiba ya Utekelezaji ya Shughuli za Uchaguzi Mkuu, kikao hiki kilipangwa kufanyika mwanzoni mwa mwezi Oktoba, lakini kutokana na jukumu la maandalizi na usimamizi wa Mitihani ya Darasa la Saba ambalo pia linawahusu ninyi moja kwa moja Tume iliona ni vema kusogeza mbele tarehe ya mkutano huu kupisha zoezi hilo muhimu la Kitaifa.

Mkutano huu umeandaliwa katika kanda tano ili kuwapunguzia umbali wa kusafiri kutoka katika maeneo yenu hivyo kuokoa muda katika kipindi hiki cha maandalizi.

**Ndugu washiriki**

Nachukua nafasi hii kuwakaribisha katika mkutano huu ikiwa ni mwendelezo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kukutana nanyi katika kipindi hiki cha kuelekea tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Lengo ni kukumbushana masuala muhimu yatakayosaidia kufanikisha zoezi la Uchaguzi Mkuu.

**Ndugu washiriki**

Tume ilikutana na Wasimamizi wa Uchaguzi Jijini Dodoma tarehe 24 Agosti, 2020 ambapo mada mbalimbali zinazohusu Usimamizi na Uendeshaji wa Uchaguzi ziliwasilishwa. Tume pia, iliandaa mafunzo kwa ajili yenu yaliyofanyika kati ya tarehe 27 Julai, 2020 na hadi tarehe 04 Agosti, 2020 katika vituo 14.

Aidha, Tume imewapatia Sheria, Kanuni, vijitabu vya Maelekezo mbalimbali na Mambo Muhimu ya Kuzingatia ili yawaongoze katika utekelezaji wa majukumu yenu ya kiuchaguzi. Vilevile, mlipatiwa *checklists na* Ratiba ya Utekelezaji ya Shughuli za Uchaguzi Mkuu 2020 inayoonesha shughuli zote muhimu ambazo mnatakiwa kuzitekeleza. Ni matarajio ya Tume kuwa hadi kufikia kipindi hiki tayari mmeyaelewa vema majukumu yenu na namna yanavyotakiwa kutekelezwa. Tume inawakumbusha kurudia tena kusoma Maelekezo yote yaliyotolewa na Tume ili kujikumbusha taratibu zote za mchakato wa uchaguzi. Hii itasaidia kuendesha Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 kwa weledi na ufanisi zaidi. Kushindwa kutekeleza majukumu yenu ipasavyo kutasababisha malalamiko na kupelekea uvunjifu wa amani.

**Ndugu Washiriki,**

Baada ya kukamilika kwa zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga kura kwa awamu zote mbili kama ilivyo matakwa ya kisheria,

Daftari hili kwa sasa lina jumla ya Wapiga Kura wapatao milioni **29,188,347.** Aidha, kwa upande wa Tanzania Zanzibar Tume hutumia Daftari la Wapiga Kura lililoandaliwa na Tume ya Taifa ya Zanzibar.

Katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu kutakuwa na vituo **81,567** vya kupigia kura kwa nchi nzima. Mmeletewa orodha ya vituo vya kupigia kura vilivyopo katika maeneo yenu. Pia, mmeletewa nakala mbili za orodha za wapiga kura na nakala moja ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa kila kutuo cha kupigia kura kwa madhumuni ya kutumika katika mchakato wa uchaguzi kama mlivyoelekezwa kwenye mafunzo.

**Ndugu Washiriki**

Tume inafahamu kuwa mmepewa maelekezo ya ujenzi wa vituo katika maeneo ya wazi. Mnasisitizwa kuzingatia maelekezo hayo na ujenzi huo uzingatie idadi ya mawakala, watendaji wa uchaguzi na eneo la kuweka kituturi ili mpiga kura aweze kupiga kura yake kwa siri.

Aidha, inapotokea hitaji la kuhamisha kituo cha kupigia kura muhakikishe mnawatangazia wananchi eneo husika na pia vyama vya vyote vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi vinaarifiwa.

Vilevile, miongoni kwa vifaa mlivyopokea kutoka Tume yapo mabango mshale makubwa na madogo. Mabango mshale yabandikwe kwenye njia kuu zinazoelekea vituoni kuonesha mahali vituo vilipo.

**Ndugu Washiriki**

Hadi tarehe ya leo Tume inafahamu kwamba imeshawatumia sehemu kubwa ya vifaa vinavyohitajika kwa ajili ya kufanikisha uchaguzi katika maeneo yenu. Vifaa mlivyoletewa ni pamoja na vile muhimu kama vile karatasi za kura. Mnaelekezwa kuhakiki vifaa vyote kuona kama ni sahihi na idadi inatosheleza mahitaji na vihifadhiwe katika sehemu salama hadi siku ya uchaguzi. Vilevile, vifaa hivyo vipangwe kwa kila kituo kwa ajili ya kugawanywa tayari kwa kukabidhiwa kwa Wasimamizi wa Vituo tarehe 27 Oktoba, 2020.

**Ndugu Washiriki,**

Kwa mujibu wa Ratiba ya utekelezaji wa Shughuli za Uchaguzi Mkuu mchakato wa kuwapata Watendaji wa Vituo vya kupigia kura ulianza tarehe 21 Septemba, 2020. Ni imani ya Tume kuwa wote mmefanya kazi hiyo kwa weledi na uadilifu ili kupata watendaji wenye uwezo watakaofanya kazi hivyo vizuri. Ni Imani yangu mmekamilisha mchakato huo. Kwa halmashauri ambazo bado, mnasisitizwa kukamilisha kazi hiyo mapema kabla ya tarehe iliyopangwa kwa ajili ya mafunzo. Aidha, mnakumbushwa kufanya mawasiliano mapema na Makamanda wa Polisi wa Wilaya kwa ajili ya kupata walinzi wa vituo wa kutosha.

**Ndugu Washiriki**

Kuanzia tarehe 24 hadi tarehe 26 Oktoba, 2020 mtatakiwa kutoa mafunzo kwa Wasimamizi wa Vituo, Wasimamizi Wasaidizi wa Vituo na Makarani Waongozaji. Mnatakiwa kuyapa umuhimu mkubwa na wa pekee mafunzo hayo hasa ikizingatiwa kuwa watendaji mtakao wafundisha ndio watakao simamia zoezi la upigaji kura na kuhesabu kura vituoni. Mnasisitizwa pia kufanya mafunzo kwa hasa kujaza fomu zote zikiwepo za matokeo ya uchaguzi ili kupunguza makosa yanayoweza kujitokeza kutokana na kutozielewa vizuri fomu hizo.

**Ndugu Washiriki,**

Tarehe 21 Oktoba, mnatakiwa kuwaapisha mawakala wa vyama vya siasa. Mnasisitizwa kuvitaka vyama vya siasa kuwasilisha orodha ya mawakala wao mapema. Tume inawasisitiza Wasimamizi wote wa Uchaguzi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi wanaohusika katika kuapisha Mawakala, kuandaa utaratibu mzuri utakaorahisisha zoezi la kuwaapisha mawakala hao katika namna ambayo haitasababisha malalamiko.  Mawakala hao waapishwe kwenye ngazi ya kata ili kupunguza msongamano katika ngazi ya majimbo.

**Ndugu Washiriki**

Tarehe 28 Oktoba, 2020 ndio **siku ya kupiga kura**. Vituo vinatakiwa kufunguliwa saa 1.00 asubuhi kama inavyoelekezwa na Tume.

Watendaji wa vituo waelekezwe kuwahi vituoni mapema ili wafanye maandalizi. Baada ya wapiga kura kupiga kura zao wanatakiwa kuondoka vituoni.

**Ndugu wa Shiriki**

Kwa kumalizia niwakumbushe kuwa, kwa kuzingatia kifungu cha 89A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 88A cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume haitasita kumchukulia hatua Msimamizi wa Uchaguzi yeyote atakayefanya kwa makusudi vitendo vitakavyosababisha uchaguzi kuharibika katika jimbo au kata. Aidha, atakayesababisha matokeo ya uchaguzi kutenguliwa na mahakama baada ya uchaguzi kwa kutozingatia maelekezo ya Tume na kuisababishia serikali hasara ya kurudia uchaguzi (by-election) atatakiwa kufidia hasara hiyo kwa mujibu wa kifungu cha 89B cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu 88B cha Sheria za Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 na Sheria ya The Public Officers, (Recovery of Debts) Act, Cap. 76.

Baada ya kusema hayo, sasa napenda kutamka rasmi kuwa mkutano umefunguliwa.

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**